

FUNDISHO LA BIBLIA KUHUSU

# Roho Mtakatifu

*Je, Waadventista wa Sabato Hawakukosea?*

Mch. Almodad Amos Yaragwiller

FUNDISHO LA BIBLIA KUHUSU

# Roho Mtakatifu

*na Mch. Almodad Amos*

# Asomaye na Afahamu

**Haiwezekani Kufahamu, Mpaka Kwanza Umesoma au umesikia kutoka kwa aliyesoma Neno la Bwana**

Mathayo 24:15; Warumi 10:17

Haki zote zimehifadhiwa. Unaruhusiwa kusambaza kwa njia ya kidijitali lakini sio kuuza kwa namna yoyote ile bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa kitabu hiki. Ukihitaji nakala iliyochapishwa wasiliana na mwandishi kwa
+255718834621 | modaofpeace@gmail.com

# Yaliyomo

**YALIYOMO**....................4

**UTANGULIZI**....................5

**MUHTASARI WA KILE TUNACHOAMINI**.................... 5

**MAANA YA NENO ROHO KATIKA BIBLIA?**....................6
- **Maana ya Neno "Roho" Katika Lugha Asilia**....................6
- **Matumizi ya Neno "Roho" Katika Biblia**....................6
- **Muhtasari wa Maana ya Neno Roho**....................8

**ROHO MTAKATIFU NI NANI?**....................9
- **Majina ya Roho Mtakatifu Katika Biblia**....................9
- **Sifa za Mungu**....................11
  - A) Sifa za Mungu Zisizohamishika....................11
  - B) Sifa za Roho Mtakatifu....................12
- **Kazi za Roho Mtakatifu**.................... 13

**VIASHIRIA VYA UWEPO WA ROHO MTAKATIFU MAISHANI**....................18

**NINAWEZAJE KUMPATA ROHO MTAKATIFU MAISHANI?**....................21
- **Nini Maana ya Kumpokea Roho Mtakatifu?**....................22
- **Namna ya Kuendelea Kuwa Roho Mtakatifu**....................22

**NUKUU ZA ROHO YA UNABII JUU YA ROHO MTAKATIFU**....................24

**REJEA**....................25

# MUNGU ROHO MTAKATIFU

## UTANGULIZI

Waadventista wa Sabato tunaiona Biblia ikiwa imegawanyika katika Mafundisho Makuu Sita ya Biblia. Somo hili la Roho Mtakatifu linaingia katika kundi la Mafundisho ya Biblia yanayoitwa Mafundisho Kuhusu Mungu au Kitaalam Teolojia. Katika kundi hili la Mafundisho Kuhusu Mungu yapo masomo/mada tano ambazo kwa kawaida tunaziita Imani za Msingi; Imani hizo za Msingi ni: 01) Maandiko Matakatifu 02) Utatu Mtakatifu 03) Mungu Baba 04) Mungu Mwana, na 05) Mungu Roho Mtakatifu. Hapa hatutajifunza Imani za Msingi zote tano, bali tutajikita katika Imani ya Msingi namba 05 inayoitwa Mungu Roho Mtakatifu. Miongoni mwa mambo tutakayojifunza katika somo hili ni pamoja na haya:

- Kile tunachoamini Waadventista wa Sabato juu ya Roho Mtakatifu.
- Maana ya neno roho katika Biblia
- Sifa za Roho Mtakatifu
- Matendo au kazi za Roho Mtakatifu
- Namna ya kutambua kuwa Mtu anaye Roho Mtakatifu.
- Namna mtu anavyoweza kumpata Roho Mtakatifu
- Kile Roho ya Unabii inachosema Kuhusu Roho Mtakatifu

Ni imani yangu kuwa utakuwa na wakati mzuri katika safari hii makini ya muhimu ya fundisho kuhusu Roho Mtakatifu. Wakati wote unapojifunza Maandiko Matakatifu kumbuka sana jambo hili: "Kamwe pasiwe na kujifunza Biblia bila kuwa na maombi.[1]"

## MUHTASARI WA KILE TUNACHOAMINI

Mungu Roho Mtakatifu ni wa milele, amekuwa mtendaji pamoja na Baba na Mwana katika Uumbaji, katika Yesu kufanyika mwili na katika ukombozi. Aliwavuvia waandishi wa Maandiko Matakatifu. Aliyajaza maisha ya Yesu Kristo na uwezo. Huwavuta na kuwasadikisha wanadamu; na wale wanaoitikia huwafanya upya na kuwarejesha katika sura ya Mungu. Alipelekwa na Baba na Mwana ili kuwa siku zote pamoja na watoto wake, hueneza karama za Roho kwa kanisa, huwapa uwezo wa kumshuhudia Kristo, na kwa ulinganifu na Maandiko Matakatifu hongoza katika kweli yote.

Kwa ufupi kabisa, hivyo ndivyo Waadventista wa Sabato tunavyoamini kuhusiana na fundisho la Roho Mtakatifu, na kutokana na kile tunachokiona katika maandiko matakatifu, yaani Biblia na Roho ya Unabii kwa Ujumla.

1 White, E. G. (1911). The Great Controversy Between Christ and Satan (p. 599). Pacific Press Publishing Association

## MAANA YA NENO ROHO KATIKA BIBLIA?

Jina Roho Mtakatifu ni jina ambalo limezua mijadala mingi ya kiteolojia kwa sababu ndani ya jina hilo kuna neno “Roho” ambalo linamaana nyingi na matumizi mengi sana katika Biblia. Kabla ya kuangalia matumizi ya neno Roho ndani ya Biblia, ni muhimu kujua maana ya neno Roho kama linavyofafanuliwa katika kamusi mbalimbali zinazoonyesha maana ya maneno ya Kiebrania, Kiyunani na Kiaramu ambazo ni lugha tatu walizozitumia Manabii, Mitume na Yesu mwenyewe katika kutoa mafunuo ambayo leo hii yanajulikana kama Biblia.

### *Maana ya Neno “Roho” Katika Lugha Asilia*

Lugha zilizotumika kuandika Sehemu ya Biblia inayojulikana kama Agano la Kale ni lugha ya Kiebrania na lugha ya Kiaramu. Katika lugha zote (hizo mbili) neno ambalo kwa Kiswahili hufasiriwa kama Roho ni neno **rûaḥ** (kiebrania: רוּחַ). Katika lugha ya Kiyunani ni neno **pneuma** (Kiyunani: ***πνεῦμα***).

Kando ya maana zitakazoongezeka kutokana matumizi ya neno hilo katika Biblia, neno “roho” katika Kiebrania, Kiaramu na Kiyunani kwa asili humaanisha: Upepo, Hewa au Pumzi.

### *Matumizi ya Neno “Roho” Katika Biblia*

Neno “Roho” ni neno linalojitokeza takribani mara 765 katika Biblia ya Kiswahili cha Kimvita, toleo la Union Version, ambalo wasomaji wengi wa Biblia za Kiswahili hulitumia. Neno “roho” linajitokeza mara 386 katika Agano la Kale na mara 379 katika agano Jipya.

Neno hili linazo maana kadhaa ambazo mtu aweza kuzitambua kulingana na muktadha wa aya husika ambapo neno hilo limetumika. Kabla hatujajifunza fundisho la Roho Mtakatifu, ni muhimu kutambua jinsi neno “Roho” linavyotumika katika Biblia, ili kuepukana na kosa la kuchukua maana isiyokusudiwa na kuitumia maana hiyo mahali ambapo halikukusudiwa kutumika. Zifuatazo ni maana za neno Roho Katika Biblia pamoja na mifano michache:

**01. Roho ni Nguvu ya Uhai Inayomuwezesha mwanadamu kuwa Nafsi hai.**

Hii ni Pumzi ambayo Mungu alimpulizia mwanadamu puani. Mfano wa matumizi ya neno hili katika Biblia ni wakati Mungu alipompulizia mwanadamu Pumzi ya Uhai puani. Kitendo cha kumpulizia puani mwanadamu pumzi ya uhai, kilimpatia mwanadamu kuwa kiumbe hai. Hiyo pumzi ambayo Mungu alimpulizia mwanadamu puani inaitwa “roho” katika kitabu cha Ayubu 27:3. Linganisha aya hizi za Biblia tafadhali

> BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, **akampulizia puani pumzi ya uhai**; mtu akawa nafsi hai.
> **~ Mwanzo 2:7**
>
> (Kwa kuwa uhai wangu ukali mzima ndani yangu, Na **roho ya Mungu i katika pua** yangu;)
> **~ Ayubu 27:3**

## 02. Roho humaanisha Mtu, Utu wa Ndani, Mawazo au Akili

Yapo matumizi kadhaa ambayo yanaonyesha neno roho linamaanisha mtu katika ukamilifu wake, au linamaanisha utu wa ndani kwa maana ya tabia flani au linamaanisha akili ya mtu:

### *a) Neno "roho" linamaanisha mtu katika ukamilifu wake yaani mwanadamu.*

**Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa**; mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe, haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake.

**~ Ezekieli 18:20**

### *b) Neno "roho" linamaanisha utu wa ndani yaani akili au wazo*

Je! Ni nani aliyetia hekima moyoni? Au ni nani aliyetia **ufahamu rohoni**?

**~ Ayubu 38:36**

Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu, bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya **siri katika roho yake**.
**~ 1 Wakorinto 14:2**

Naye huyo mwanamke alikuwa na **uchungu rohoni mwake**, akamwomba Bwana akalia sana.

**~ 1 Samueli 1:10**

Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu, bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya **siri katika roho yake**.

**~ 1 Wakorinto 14:2**

### *c) Neno "roho" linamaanisha tabia*

Heri mwisho wa neno kuliko mwanzo wake, Na **mvumilivu rohoni** kuliko mwenye **roho ya kiburi**.
**~ Mhubiri 7:8**

Afadhali kuwa na **roho ya unyenyekevu** pamoja na maskini, Kuliko kugawanya nyara pamoja na wenye kiburi.
**~ Mithali 16:19**

## 03. Neno "Roho" Humaanisha Mungu, Shetani, Malaika au Maisha ya Kiimani

### *a) Neno Roho linasimama kwa ajili ya Nafsi ya Tatu ya Mungu.*

Basi **Roho** anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani;

**~ 1 Timotheo 4:1**

Nabii Ellen anafafanua kwa  uwazi kuwa huyu Roho Mtakatifu ni Nafsi:

Tunahitaji kutambua kwamba **Roho Mtakatifu ni nafsi**, kama Mungu alivyo nafsi, naye yu atembea katika viwania hivi.
**~ Ellen G. White, Manuscript 66, 1899**

***b) Katika aya hii, katikati ya sentensi neno "roho" linaonekana tena kwa mara ya pili na safari hii linamaanisha Mashetani au Roho Wachafu (Roho zidanganyazo).***

..... wakisikiliza **roho** zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani;
**~ 1 Timotheo 4:1**

***c) Neno roho linaweza likatumika kumaanisha Malaika.***

13 Je! Yuko malaika aliyemwambia wakati wo wote, Uketi mkono wangu wa kuume Hata nitakapoweka adui zako chini ya nyayo zako? 14 Je! Hao wote si **roho watumikao**, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu?
**~ 1 Waebrania 1:13 - 14**

***d) Katika Biblia kuna wakati neno rohoni linamaanisha aina flani ya mtindo wa maisha ya Kiimani, maisha ya Ucha Mungu, Maisha ya Kiimani au Maisha ya Kumtumaini na Kuongozwa na Roho Mtakatifu.***

Lakini mtu **wa rohoni** huyatambua yote, wala yeye hatambuliwi na mtu.
**~ 1 Wakorinto 2:15**

## *Muhtasari wa Maana ya Neno Roho*

Neno "Roho" ni neno ambalo tumeona linamaana nyingi ikiwemo pumzi ya uhai; linamaanisha Mtu; roho humaanisha Utu wa ndani yaani wazo au akili; Neno roho humaanisha tabia; Tumeona neno Roho linaweza kumaanisha nafsi ya tatu ya Mungu na wakati mwingine neno hilo hilo roho linaweza likamaanisha mashetani au malaika wema.

**Maana husika ya matumizi ya neno roho, huamuliwa na muktadha. Muktadha ni kuchungaza maana ya neno au aya au sura ya Biblia kwa kuzingatia maana aliyoikusudia mwandishi wa Biblia katika mazingira yaliyokuwepo wakati akiandika sehemu flani ya maandiko.**

## ZINGATIA

**Katika sehemu zote za somo hili zilizosalia, tutakapo kuwa tukisema Roho au Roho Mtakatifu, tutakuwa tukizungumza na kujifunza habari za Nafsi ya Tatu ya Mungu, isipokuwa mahali ambapo itaelekezwa vinginevyo.**

## ROHO MTAKATIFU NI NANI?

Moja kati ya mambo ambayo yamekuwa yakileta mtanziko mkubwa katika kujifunza maandiko ni habari ya utambulisho wa Roho Mtakatifu kwa wanadamu.

Yesu Kristo akiongelea habari za kujulikana kwa Roho Mtakatifu alisema wale wanaomtambua Roho Mtakatifu ni wale ambao Roho Mtakatifu anakaa kwao.

> ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi **mnamtambua, maana anakaa kwenu**, naye atakuwa ndani yenu.
>
> **~ Yohana 14:17**

Kwa maneno mengine, huwezi kumuelewa Roho Mtakatifu kwa kutumia akili zako mwenyewe na kwa uchunguzi wako mwenyewe bila kwanza kuwa na Roho Mtakatifu ndani yako. Ili umuelewe ni lazima awe ndani yako kwanza.

Na hivyo ni muhimu sana katika kujifunza maandiko haya uendelee kuomba kwamba Mungu akupatie Roho Mtakatifu ili akae kwako na hatimaye upate kumtambua kwamba Yeye ni nani. Ahadi ya Yesu ni kwamba wale watakaompokea Roho Mtakatifu maishani mwao ndio watakaoweza tu kumtambua.

**Mungu huwa anajifunua kwetu kuhusu jinsi alivyo kwa kutumia matendo yake, sifa zake na kwa kutumia majina yake. Ni lazima twende kwenye sifa Zake na kisha tuyaangalie matendo yake.**

### *Majina ya Roho Mtakatifu Katika Biblia*

Roho Mtakatifu anayo majina kadha wa kadha ambayo yanaonekana katika Maandiko Matakatifu. Jina moja linaweza kubeba sifa kadhaa za Mungu au laweza kubeba sifa moja ambayo hutusaidia kuona jinsi Mungu anavyojifunua kwetu. Kwa Mfano: Biblia inamuita Mungu Mwamba (katika Kumb. 32:4) huwezi kuhitimisha kwa kutumia jina hilo moja na kusema Mungu ni jabali. Hilo jina linafunua sifa zake kwamba Mungu yu Imara na anaweza kutegemewa, Yeye halegei, n.k. Huwezi kwa kutumia jina hilo moja ukasema Mungu ni Jabali. Hali kadhalika katika majina ya Roho Mtakatifu tutakayoyaona, tutagundua kuwa majina hayo huonyesha sifa zake lakini jina moja halitoshi kumaanisha kwa ukamilifu jinsi alivyo na ndiyo maana maandiko yanatufunulia majina kadha wa kadha yanayomuhusu. Majina hayo ni:

#### Anaitwa Roho wa Yesu

> Walipofika kukabili Misia wakajaribu kuenda Bithinia, lakini **Roho wa Yesu** hakuwapa ruhusa,
>
> **~ Matendo 16:7**

### Anaitwa Roho wa Mwanawe/Mwana

Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma **Roho wa Mwanawe** mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba.

**~ Wagalatia 4:6**

### Anaitwa Roho wa Mungu; Pia anaitwa Roho wa Kristo

Lakini ikiwa **Roho wa Mungu** anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na **Roho wa Kristo**, huyo si wake.

**~ Warumi 8:9**

### Anaitwa Roho wa Yesu Kristo

Maana najua ya kuwa haya yatanigeukia kuwa wokovu wangu, kwa sababu ya kuomba kwenu, na kuruzukiwa **Roho wa Yesu Kristo**;

**~ Wafilipi 1:19**

### Anaitwa Msaidizi

Nami nitamwomba Baba, naye atawapa **Msaidizi** mwingine, ili akae nanyi hata milele;

**~ Yohana 14:16**

### Anaitwa Roho Mtakatifu

Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na **Roho Mtakatifu** ambaye Mungu amewapa wote wamtiio.

**~ Matendo 5:32**

### Anaitwa Roho wa Mungu

Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila **Roho wa Mungu**.

**~ 1 Wakorintho 2:11**

### Anaitwa Roho wa Neema

Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kumfanyia jeuri **Roho wa neema**?

**~ Waebrania 10:29**

### Anaitwa Roho

Basi **Roho** anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani;

**~ 1 Timotheo 4:1**

### Anaitwa Mungu

3 Petro akasema, Anania, kwa nini Shetani amekujaza moyo wako **kumwambia uongo Roho Mtakatifu**, na kuzuia kwa siri sehemu ya thamani ya kiwanja? 4 Kilipokuwa kwako, hakikuwa mali yako? Na kilipokuwa kimekwisha kuuzwa, thamani yake haikuwa katika uwezo wako? Ilikuwaje hata ukaweka neno hili moyoni mwako? **Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu**.
**~ Matendo ya Mitume 5:3, 4**

### Anaitwa Bwana

25 Na walipokuwa hawapatani wao kwa wao, wakaenda zao, Paulo alipokwisha kusema neno hili moja, ya kwamba, **Roho Mtakatifu alinena** vema na baba zetu, kwa kinywa cha nabii Isaya, 26 akisema, Enenda kwa watu hawa, ukawaambie, Kusikia, mtasikia wala hamtafahamu; Na kuona, mtaona wala hamtatambua;
**~ Matendo ya Mitume 28:25, 26**

8 Kisha **nikaisikia sauti ya Bwana, akisema**, Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi. 9 Naye akaniambia, Enenda, ukawaambie watu hawa, Fulizeni kusikia, lakini msifahamu; fulizeni kutazama, lakini msione. 10 Uunoneshe moyo wa watu hawa, ukayatie uzito masikio yao, ukayafumbe macho yao; wasije wakaona kwa macho yao, na kusikia kwa masikio yao, na kufahamu kwa mioyo yao, na kurejea na kuponywa.
**~ Isaya 6:8 - 10**

Neno Bwana katika Isa. 6:8 ni (**אֲדֹנָי** –ʾ**ăḏō·nāy**): Adonay ni Jina la Mungu wa Kweli wa Biblia, jina hilo linaloonyesha mamlaka yake na fahari ya juu sana ya Mungu.

## *Sifa za Mungu*

Moja kati ya mambo ambayo tuliyaona hapo awali ni kwamba Mungu huwa anajifunua kwetu na kutuonyesha namna alivyo kwa kutumia sifa Zake. Sifa za Mungu zinagawanyia katika makundi makubwa mawili; kuna sifa zinazohamishika ambazo hizo ni tabia ambazo anaweza kuvipatia viumbe vyake kuwa nazo, na kisha kuna sifa zisizohamishika ambazo hizo ni sifa zisizoweza kupatikana ndani ya viumbe. Hebu na tutazame sifa za Mungu Zisizohamishika, kwa Ujumla wake, na kisha tutazame sifa za Roho Mtakatifu:

### *A) Sifa za Mungu Zisizohamishika*

- Mungu yupo pasipo kuumbwa, anao uzima ndani yake (Yoh. 5:26).
- Yu huru kuradhi chochote kwa mapenzi yake (Efe. 1:5).
- Katika uwezo (Zab.115:3).
- Mungu anajua vyote (Ayu.37:16; Zab.139:1-18; 147:5; 1Yoh.3:20). Kwa sababu Yeye ni Alfa na Omega (Uf.1:8) anaujua mwisho tangu mwanzo (Isa.46:9-11).
- Mungu hupatikana wakati wote na mahali pote (Zab.139:7-12; Ebr.4:13), akipita anga za juu, wakati huo huo akiwa ndani ya kila kitu kwenye anga.
- Mungu ni wa milele (Zab.90:2; Uf.1:8), akivuka vikomo vya wakati, na wakati huo huo akiwamo katika kila kipengele cha wakati.
- Mungu anao uwezo wote. Yaani, hakuna kinachoshindikana kwake hututhibitishia kuwa chochote anachokikusudia, hukifanya (Dan. 4:17; 25, 35; Mt. 19:26; Uf.19:6).

## *B) Sifa za Roho Mtakatifu*

### Roho Mtakatifu ni wa Milele

basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa **Roho wa milele** alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?

**~ Waebrania 9:14**

Hakuna awezaye au kiwezacho kuwa cha milele isipokuwa Mungu tu. Roho Mtakatifu maandiko yanaonyesha ni wa Milele. Hii ni sifa ya Mungu, kwa hiyo Roho Mtakatifu ni Mungu.

### Roho Mtakatifu ni Mtakatifu

Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa **Roho Mtakatifu**.

**~ Mathayo 1:20**

**Hakuna aliye mtakatifu** kama BWANA; Kwa maana hakuna ye yote ila wewe, Wala hakuna mwamba kama Mungu wetu.

**~ 1 Samweli 2:2**

Jina la Roho limeambatana na neno Mtakatifu. Hilo jina Mtakatifu linaonyesha jinsi Mungu alivyo Mtakatifu na pia ni Jina la Mungu peke yake. Huwezi ukakuta mtu anaitwa Mtakatifu au malaika anaitwa Mtakatifu. Ukiona nafsi flani inaitwa Mtakatifu, hiyo haina maana nyingine isipokuwa Mungu.

### Roho Mtakatifu Anajua Mambo Yote Hata na Mafumbo ya Mungu

Je! Wewe hukujua? Hukusikia? Yeye Mungu wa milele, Bwana, Muumba miisho ya dunia, hazimii, wala hachoki; **akili zake hazichunguziki**.

**~ Isaya 40:28**

Ee Bwana, jinsi yalivyo makuu matendo yako! **Mawazo yako ni mafumbo makubwa**.

**~ Zaburi 92:5**

Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. **Maana Roho huchunguza yote**, hata **mafumbo ya Mungu**.

**~ 1 Wakorintho 2:10**

Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu **hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu**.

**~ 1 Wakorintho 2:11**

Aya hizi zinaonyesha Roho Mtakatifu anajua mambo yote mpaka na mambo ambayo ni mafumbo ya Mungu. Biblia inasema mafumbo ya Mungu ni Mawazo yake. Kwa hiyo kama Roho anayajua mawazo ya Mungu, hakuna mashaka kuwa Roho Mtakatifu si nguvu wala kitu kingine bali ni Mungu, tena mwenye ufahamu wote au ujuzi wote.

### Roho Mtakatifu ni Muumbaji

**Mikono yako imeniumba na kunifinyanga**; Nawe utageuka na kuniangamiza?
**~ Ayubu 10:8**

**Roho ya Mungu imeniumba**, Na pumzi za Mwenyezi hunipa uhai.
**~ Ayubu 33:4**

Wakati Mungu akisema na tumfanye mtu kwa sura yetu na kwa mfano wetu (Mwa. 1:26), Roho Mtakatifu alikuwepo na maandiko yanasema ndiye aliyetufinyanga kwa sababu Ayubu 10:8 anasema "mikono ya Mungu imeniumba" na kunifinyanga na kitu hicho hicho kinazungumzwa katika 33:4 anaposema "Roho yako imeniumba." Hakuna awezaye kuwa Muumbaji isipokuwa Mungu tu.

### Roho Mtakatifu Yuko Kila Mahali

Niende wapi nijiepushe na **roho yako**? Niende wapi niukimbie uso wako? 8 Kama ningepanda mbinguni, Wewe uko; Ningefanya kuzimu kitanda changu, Wewe uko.

**~ Zaburi 139:7, 8**

Hakuna awezaye au kiwezacho kuwa cha milele isipokuwa Mungu tu. Roho Mtakatifu maandiko yanaonyesha yeye ni wa Milele.

## *Kazi za Roho Mtakatifu*

Lakini huyo **Msaidizi**, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, **atawafundisha yote**, na **kuwakumbusha yote niliyowaambia**.

~Yohana 14:26

Neno ambalo kwa lugha ya Kiswahili limefasiriwa kama "Msaidizi" kwa lugha ya kiyunani ni neno **paraklētos**. Kitenzi cha neno **paraklētos** ni **parakaleō** ambacho ingawa kimefasiriwa kama "**mfariji**" mara 23 katika Agano Jipya, neno hilo pia limefasiriwa kama "**mshawishi**" mara 19[2]" katika Agano Jipya.

Pia, neno **paraklētos** limeundwa kwa kuunganisha maneno mawili, kuna neno **para**, (kiambishi awali) ikiwa na maana ya "**kando**," na kisha kuna kivumishi "**klētos**," kinachomaanisha "kuitwa," au "aliyeitwa." Kwa hiyo neno "**paraklētos**" linamaanisha "yeye aliyeitwa kusimama kando ya.[3]"

Ni jambo lenye baraka kiasi gani leo hii kujua kuwa Roho Mtakatifu anasimama kando yetu. Kila mmoja wetu anahitaji Roho Mtakatifu asimame kando yake maana katika dunia iliyojaa shida na mateso ya kila namna hatuwezi kustahimili tukiwa peke yetu. Upande mmoja kuna majaribu ya dhambi, upande mwingine kuna huzuni na machozi yatokanayo na matatizo ya kila namna ya ulimwengu huu; lakini habari njema ni kwamba, yuko Roho Mtakatifu asimamaye kando ya watu wa Mungu. Kamwe hatujawahi kuwa peke yetu: Maana wakati Dunia ilipoanguka dhambini Yesu alikuja na akaitwa jina lake Imanueli, yaani Mungu

2 Nichol, F. D., ed. (1980). The Seventh-day Adventist Bible Commentary (Vol. 5, p. 1037). Review and Herald Publishing Association.

3 Ibid

alikuwa pamoja nasi. Kamwe hatujawahi kuwa peke yetu:  Maana baada ya dhambi kuwa imepita na tutakapoingia katika Yerusalemu mpya, maandiko yanasema "Mungu mwenyewe atakuwa pamoja na watu wake" (Ufu. 21:3). Hatujawahi kuwa peke yetu kwa sababu  wakati Yesu alipokuwa akipaa kwenda mbinguni alisema nitawaachia "Msaidizi" na huyo msaidizi ndiye asimamaye kando yetu ya sasa.

Roho Mtakatifu anaitwa msaidizi maana yuko karibu na sisi ili apate kutupatia msaada katika mambo kadhaa kama maandiko yanavyozifunua kazi zake kwetu. Zifuatazo ni kazi za Roho Mtakatifu:

## Kutufundisha Kweli Yote na Kutukumbusha Maneno ya Mungu

> Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, **atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote** niliyowaambia
>
> **~ Yohana 14:26**

Moja kati ya majukumu makubwa kabisa ambayo Roho Mtakatifu huyafanya ni kutufundisha yote na kutukumbusha yote aliyotuambia Yesu.

Katika maisha haya, Roho Mtakatifu hutufundisha kuishi kwa kadri ya maneno tunayojifunza kwenye neno la Mungu. Ndiyo ambaye hutwambia usifanye hivi na hivi au fanya hivi na hivi, akirejea yale tuliyoyasoma au kuyasiki katika neno.

Wakati mwingine tunasoma maandiko na ndipo unashangaa kwamba mambo ambayo ulikuwa unayafahamu au ulikuwa huyaelewi kabisa, yanafunuliwa kwako kwa mtazamo mwingine kabisa na unapata maana ya maandiko ambayo hapo awali hukuwa nayo. Ni kwa sababu Roho Mtakatifu yu kando yetu ili apate kutufundisha. Anafanya kazi ya kutufundisha ili tuelewe na kuyajua yatupasayo kutenda.

> Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa.
> **~ Yohana 16:12**
>
> Lakini yeye atakapokuja, **huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote**; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.
>
> **~ Yohana 16:13**

Ukweli ni kwamba Yesu alitufundisha na kutufunulia mengi lakini si yote yalieleweka katika wakati wake. Mengine yalibaki kuwa mafumbo makubwa kwa watu wake. Anachotufundisha hapa ni kwamba Mafunuo ya kulielewa neno la Mungu huja kwa ngazi na hatua tofauti tofauti. Maandiko yanaonyesha kweli yote haiji kwa mara moja bali Roho Mtakatifu huikamilisha hatua kwa hatua. Kazi ya Roho Mtakatifu ni kutuongoza mpaka tutakapoielewa kweli yote. Nuru ya neno la Mungu hukua ndani yetu na ndiyo maana uelewa wa maandiko hupanuka siku kwa siku (Dan. 12:4).

## Hugawa na Kutoa Karama; na Kuwezesha Huduma za Kiroho Zifanyike

Basi pana tofauti za karama; bali Roho ni yeye yule.
**~ 1 Wakorintho 12:4**

Tena pana tofauti za huduma, na Bwana ni yeye yule.
**~ 1 Wakorintho 12:5**

lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, **akimgawia kila mtu** peke yake kama apendavyo yeye.
**~ 1 Wakorintho 12:11**

Ukianza kusoma katika aya ya 1 mpaka aya ya 11, utagundua kuwa Roho Mtakatifu ndiye huwafanya na kuwawezesha watu kuwa na Karama za Roho na Huduma. Karama ni vifaa ambavyo Mungu huvitoa ili kufanikisha utendaji wa kazi ya Injili na kufanikisha malezi ya kiroho ya Kanisa. Baadhi ya mambo ambayo yametajwa ambayo Roho Mtakatifu huwawezesha watu kufanya mambo hayo ni pamoja na: Kuwafanya kuwa manabii na kuwawezesha kuutoa unabii, kuwafanya watu kuwa na hekima, na wengine huwapa maarifa, wengine Imani, wengine uponyaji, wengine matendo ya miujiza, wengine unabii, wengine kupambanua roho, wengine aina za lugha na wengine tafsiri za lugha.

Roho Mtakatifu ndiye awapaye watu karama, na ndiye anayewawezesha kuzitumia karama hizo. Na Yeye huyo Roho hugawa karama hizi si kama anavyoelekezwa, bali kama apendavyo. Hii inatufundisha pia kuwa Roho Mtakatifu anauwezo wa kuchagua. Kitendo ha Yeye kugawa kama apendavyo huonyesha kuwa yu radhi.

## Roho Mtakatifu Huuhakikishia Ulimwengu Juu ya Dhambi, Haki na Hukumu

Naye akiisha kuja, huyo **atauhakikisha** ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu.
~ Yohana 16:8

Roho Mtakatifu anafanya kazi ya kuwahakikishia wanadamu juu ya ukweli kuhusu dhambi. Mtu anapofanya jambo ambalo linakinzana na mapenzi ya Mungu yanayofunuliwa kwetu kupitia neno la Mungu, Roho Mtakatifu hufanya kazi ya kumshawishi mtu huyo kwamba kwa mujibu wa neno la Mungu ni kweli kuna kosa limetokea ambalo ni dhambi. Roho hulifanya hilo kwa kutuonyesha haki yaani namna ambayo mtu alipaswa kuishi na kisha humuelekeza mtu kuwa endapo toba ya dhati itafanyika mtu huyo ataepukana na hukumu ya adhabu na badala yake atapata hukumu ya haki ipatikanayo kwa neema kwa njia ya Imani (Efe. 2:8).

Mtu anapojihisi kuwa mwenye dhambi, kuhitaji msaada wa kiroho dhidi ya dhambi, na anapojisikia kuchukua hatua ya kiimani ya kushughulika na dhambi; huwa haitokei kwa bahati mbaya. Huwa inatokea kwa sababu Roho Mtakatifu anaifanya kazi hiyo, ndiyo maana mtu akimkufuru na kumkataa Roho Mtakatifu mtu huyo hawezi kupata msamaha wala wokovu kwa sababu anayetusaidia kujisikia tunauhitaji wokovu ni Roho Mtakatifu. Bila Yeye, hakuna mdhambi anayeweza kuokolewa.

## Roho Mtakatifu Hufanya Iwezekane Kuishi Maisha Mapya ya Kiroho (Kuzaliwa Upya)

Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu. 6 Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na **kilichozaliwa kwa Roho ni roho***
~ Yohana 3:5, 6

Roho Mtakatifu ndiye anayewawezesha wanadamu kupata ushindi dhidi ya dhambi na kuanza kuishi maisha mapya ya Kiimani. Neno kuzaliwa kwa Roho linaashiria kuwa kiumbe kile kile kilichokuwa na maisha ya zamani, sasa kimepokea maisha mengine na si kwa maamuzi ya kiumbe bali kwa kutengenezwa na Roho Mtakatifu.

4 Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa; si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa **kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu**;
**~ Tito 3:4, 5**

Wote tunamuhitaji Roho Mtakatifu ili kuishinda dhambi na kuipata haki ya Yesu Kristo ipatikanayo kwa neema. Kuwa na Roho Mtakatifu ndani ya maisha yako ni arabuni (dhamana ya uthibitisho) kuwa hatimaye utaokolewa.

Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye **kwa yeye mlitiwa muhuri** hata siku ya ukombozi.
**~ Waefeso 4:30**

13 Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, **na kutiwa muhuri na Roho** yule wa ahadi aliye Mtakatifu.
**~ Waefeso 1:13**

Katika aya hizi, Paulo anaonyesha hatua tatu muhimu ambazo wanadamu wanaookolewa hupitia katika kupata badiliko la kitabia: “kwanza mtu husikia, kisha huamini, na kisha hutiwa muhuri juu yake[5]” kama uthibitisho kwamba mtu

* Katika Yoh 3:6 neno roho linaonekana mara mbili. Pale lilipoanza na herufi kubwa limemtaja Roho Mtakatifu, pale lilipoanza na herufi ndogo linamaanisha mtindo mpya wa maisha ya mkristo anayeishi maisha ya ucha Mungu au ya kiimani.

5 Nichol, F. D., ed. (1980). The Seventh-day Adventist Bible Commentary (Vol. 6, p. 1001). Review and Herald Publishing Association.

au watu hawa sasa “wanatambulika kama wana na binti za Mungu, walioimarishwa katika Kristo na waliwekwa wakfu kwa ajili ya kumtumikia.[6]”

Kwa hiyo, Roho Mtakatifu anafanya kazi ya kututhibitishia kuwa tumesamehewa, tumeipata haki ya Kristo kwa Imani na kwamba hatupokei hukumu ya adhabu bali ya thawabu; na hatimaye huthibitishia kuwa tumewekwa wakfu kuwa wana na binti za Mungu na kutengwa kwa ajili ya utumishi.

## Roho Mtakatifu Hufanya Utakaso Ndani Yetu na Hutuwezesha Kuwa Watii kwa Mungu

kama vile Mungu Baba alivyotangulia kuwajua katika **kutakaswa na Roho**, hata mkapata kutii na kununyiziwa damu ya Yesu Kristo. Neema na amani na ziongezwe kwenu.
**~ 1 Petro 1:2**

Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. Na **katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa**.
**~ 1 Yohana 3:24**

Utakaso ni kuwezeshwa kuishi maisha katika hali ya usafi kwa kuachana na maovu na kuishi kwa kadri Mungu anavyotaka. Mtu atajua kuwa ametakaswa kwa kipimo cha amri za Mungu. Na ndipo maandiko yanasema kwa kuzishika amri zake tutajua ya kuwa Roho Mtakatifu yuko ndani yetu. Hii hutuonyesha kuwa anayetuwezesha kuzishika amri za Mungu ni Roho Mtakatifu maana kama Yeye hayuko ndani yetu haiwezekani kuzishika amri za Mungu. Si ajabu kuona Biblia inatushauri kuendenda kwa Roho maana tukisema tuenende kwa mwili (yaani pasipo kuwa na Roho Mtakatifu), hatutaweza kuzishika amri za Mungu.

Basi nasema, **Enendeni kwa Roho**, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili.
**~ Wagalatia 5:16**

Kitu ambacho maandiko yanasisitiza hapa ni kukubali kumuomba na kumuacha Roho Mtakatifu atawale maisha yetu kwa kufuata maelekezo anayotupatia badala ya kuendelea kuishi tukipingana na uongozi wake kwa kufuata tamaa zetu wenyewe. Mtu akiishi kwa kumtegemea Roho Mtakatifu, ushindi dhidi ya dhambi ni hakika.

## Roho Mtakatifu Hutuombea

Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini **Roho mwenyewe hutuombea** kwa kuugua kusikoweza kutamkwa.
**~ Warumi 8:26**

Katika maisha haya sisi wanadamu tu wadhaifu; tunaudhaifu kwa sababu tumerithi mivuto mibaya ya kutamani kutenda dhambi na hivyo tumeathirika kwa namna ambayo hata hatujui namna ya kuhusiana na Mungu wetu kwa namna iliyokamilifu. Wakati mwingine tunajaribu kuomba ili tupate msaada wa kiroho

6 Ibid p. 833

lakini hata kuomba kwenyewe hatujui. Habari njema ni kwamba Roho Mtakatifu anatuombea kwa mahitaji yetu ya kiakili, kihisia, kimwili na kiroho pia.

### Roho Mtakatifu Huleta Ujasiri wa Kuihubiri Injili

Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote **wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri**.
**~ Matendo ya Mitume 4:31**

Lakini **mtapokea nguvu**, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; **nanyi mtakuwa mashahidi wangu** katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.
**~ Matendo ya Mitume 1:8**

Moja kati ya mambo yanayotia moyo ni kujua kuwa suala la kukamilisha utume wa Kanisa, kwa kuihubiri injili, sio suala ambalo Mungu amewaacha watu wake kulifanya wao wenyewe. Mungu ametupatia nafsi yake ya tatu ili kutupatia nguvu, ujasiri, uwezo na vipawa muimu vitakavyoliwezesha Kanisa la Mungu kukamilisha kwa uzuri kazi ya kuihubiri Injili kwa kila kiumbe.

### Roho Mtakatifu Huwaongoza na Kuwahekimisha Waaminio Katika Nyakati Ngumu

Lakini hapo watakapowapeleka, msifikiri-fikiri jinsi mtakavyosema; **maana mtapewa saa ile mtakayosema**. 20 Kwa kuwa si ninyi msemao, bali ni Roho wa Baba yenu asemaye ndani yenu.
**~ Mathayo 10:19**

Hakuna jambo linalotia moyo kama kutambua kuwa tunapokuwa katika nyakati ngumu hasa katika mateso Roho Mtakatifu huwa yuko pamoja nasi, sio tu kama mfariji, bali pia kama mshauri na mhekimishaji wetu. Yesu anasema wakati utafika ambapo watu watawatendea vibaya watu wake kwa sababu ya Imani yao. Katika wakati wa namna hiyo maandiko yanasema watu wa Mungu wataletwa katika mabaraza ili kuteswa na kuhojiwa juu ya kile wanachokiamini; katika nyakati kama hizo hatupaswi kuogopa maana maandiko yanasema Roho wa Mungu atakuwa pamoja nasi ili azungumze kupitia sisi na kupitia maneno atakayowapatia watu wake.

## VIASHIRIA VYA UWEPO WA ROHO MTAKATIFU MAISHANI

Mtu anawezaje kutambua kama Roho Mtakatifu yuko na anaendelea kufanya kazi yake ndani ya maisha ya yake? Mtu anawezaje kutofautisha kati ya matendo ya Roho wa Mungu na matendo ya roho zidanganyazo? Maswali haya ni maswali ya muhimu sana kwa sababu mara kadhaa maandiko yameonyesha Shetani akiwa na tabia ya kuigiza kazi za Mungu kwa lengo la kuwapotosha watu wa Mungu ili watu washindwe kupambanua na kujua kipi ni kipi, na mwisho kabisa awaongoze katika upotevu huku wakidhani wako salama. Ndiyo maana ni muhimu sana kujua viashiria vya uwepo wa Roho Mtakatifu maishani ili iwezekane kupambanua na kutofautisha kati ya kilicho safi na kilicho cha yule mwovu.

Pia ni muhimu sana kukumbuka kuwa ipo tofauti kati ya viashiria au dalili za mtu mwenye roho mtakatifu pamoja na ishara zitakazoambatana na watu wenye roho mtakatifu.

> Na **ishara hizi zitafuatana na hao waaminio**; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; 18 hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.
> ~ Marko 16:17

Ukichunguza kwa umakini maandiko utagundua kuwa hizo ni ishara au maajabu ambayo Mungu atayafanya ili kufanikisha kazi yake ya upelekwaji wa injili. Hayo maajabu na ishara sio kila mtu atayatenda ila wapo baadhi ya watu ambao Mungu atawawezesha kuyatenda maajabu hayo kwa faida ya kazi ya Injili/huduma:

> 4 Basi **pana tofauti za karama**; bali Roho ni yeye yule. 5 Tena **pana tofauti za huduma**, na Bwana ni yeye yule. 6 Kisha pana tofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye yule azitendaye kazi zote katika wote. 7 Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana. 8 Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho yeye yule; 9 mwingine imani katika Roho yeye yule; na mwingine karama za kuponya katika Roho yule mmoja; 10 na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri za lugha; 11 lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, **akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye**.
> ~ 1 Wakorontho 12:4 - 11

Kwa hiyo si kila mtu atapewa kunena kwa lugha, si kila mtu atapewa matendo ya miujiza, si kila mtu atakuwa nabii; maandiko yanatumia neno “wengine” kuonyesha kuwa si wote wamepewa kuwa na karama zinazofanana.

> Je! Wote ni mitume? Wote ni manabii? Wote ni waalimu? Wote wanatenda miujiza? 30 Wote wana karama za kuponya wagonjwa? **Wote wanena kwa lugha**? Wote wafasiri?
> **~ 1 Wakorinto 12:29**

Kwa hiyo basi, viashiria vya kuwepo kwa Roho Mtakatifu ni dalili ambazo mtu yeyote mwenye Roho Mtakatifu atakuwanavyo hata kama mtu huyo hakupewa baadhi ya karama za Roho. Zifuatazo ni dalili au viashiria vya mtu aliye na Roho Mtakatifu Maishani mwake:

### Kudhihirisha Tunda la Roho Maishani

Moja kati ya aya za maandiko ambazo ni maarufu sana ni Wagalatia 5. Sehemu ya sura hii inaeleza matokeo ya mtu anayeishi kwa kufuata tamaa za mwili (f.19 - 21) kisha kuanzia aya ya 22 anaeleza matokeo ya mtu anayeishi akiwa na Roho Mtakatifu ndani yake (f.22 - 23).

> 22 Lakini **tunda la Roho ni** upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, 23 upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria.
> **~ 1 Wakorintho 12:22, 23**

Kwa hiyo basi, mtu aliye Roho Mtakatifu ni mtu ambaye maisha yake yamejawa na furaha, moyoni mwake mtu huyu hujisikia kuwa na amani maana amepatanishwa na Mungu na dhambi zake zimeondolewa na kusamehewa. Mtu aliye na Roho Mtakatifu huwa na tabia ya uvumilivu; si mtu wa kukata tamaa katika imani, huwavumilia na kuwapenda wale ambao hawavumiliki, huvumilia wakati wa majaribu na hawaitupi imani yako; hao wamejaaliwa kuwa na tabia ya uvumulivu. Watu wenye Roho Mtakatifu huwa watu wema kwa viumbe vingine, kwa wageni na hata kwa maadui zao pia. Ni mtu yule aliyejaa fadhila; ni mtu yule aliye na uaminifu kama tabia yake; ni mtu mpole ambaye si mtu wa kulipa lipuka kwa hasira za hapa na pale, hata akiudhiwa hushughulika na mambo hayo kwa namna ya upole na uvumilivu. Na hatimaye mtu huyu aliyejawa na Roho Mtakatifu ni mtu ambaye anaweza kujizuia katika kula, kunywa na katika kufanya neno lolote lile ambalo linaitwa dhambi; ni mtu ambaye Mungu humsaidia kuikataa dhambi na mienendo yote mibaya. Hilo linaitwa tunda la Roho.

### Kupiga Hatua ya Katika Kuachana na Dhambi Zilizokuwa Zikikunyanyasa

Moja kati ya ushahidi mkubwa kabisa kwamba mtu anaye Roho Mtakatifu ni hali ya kupiga hatua katika maisha ya imani. Mtu anayemwamini Yesu kama Bwana na Mwokozi wa Maisha yake anatazamiwa kwamba atakua kitabia na kimwenendo. Jambo hilo haliwezekani mpaka kwanza Roho Mtakatifu amefanya kazi ndani ya mtu huyo. Hapa tunazungumzia ushahidi wa badiliko la kimaisha kutoka maisha ya zamani yasiyompendeza Mungu na kuanza kuishi maisha mapya yanayompendeza Mungu.

> si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na **kufanywa upya na Roho Mtakatifu**;
> **~ Tito 3:5**
>
> Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. Na **katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa**.
> **~ 1 Yohana 3:24**

### Kila Anayempokea Roho Mtakatifu Husikia Wito Moyoni wa Kumshuhudia Yesu

Kila mtu aliyempokea Roho Mtakatifu, hupata nguvu ya kuwaeleza wengine habari za upendo wa Mungu na habari za Yesu Kristo aliyejitoa na kufa msalabani kwa ajili ya ukombozi wa ulimwengu; mtu mwenye Roho Mtakatifu hufanywa kuwa shahidi wa Kristo.

> Lakini mtapokea nguvu, **akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu** katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.
> **~ Matendo ya Mitume 1:8**

Hakuna mtu anayebadilishwa maisha yake, ambaye hasikii msukumo wa moyoni wa kuwa na shauku ya kuwaendea wengine na kuwaeleza habari za wokovu.

### Mtu Kumpenda Mungu na Wanadamu, ni Ushahidi wa Uwepo wa Roho Mtakatifu

na tumaini halitahayarishi; kwa maana **pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yet**u na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.

**~ Warumi 5:5**

Dalili nyingine ya uwepo wa Roho Mtakatifu ni kujisikia hali ya kuwa na upendo kwa Mungu (kwa kupenda mambo ya kiroho) na kwa wanadamu wanaokuzunguka. Hali ya kutawaliwa na chuki, husuda na fitina ni dalili kuwa Roho wa Mungu bado hajapata nafasi maishani mwa mtu flani, lakini kumpenda Mungu na kuwapenda jirani zetu ni ushahidi kuwa Roho Mtakatifu anatawala katika maisha yetu.

### Kwa Kumpima Mtu Ili Kujua Ana-aina Gani ya Roho

Wapenzi, msiiamini kila roho, bali **zijaribuni hizo roho**, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani.

**~ 1 Yohana 4:1**

Katika baadhi ya nyakati kunaweza kukawa na hitaji la kupima endapo kweli mtu anaye Roho wa Mungu au hana Roho wa Mungu; hii inaweza kufanyika kulingana na madai yanayoweza kujitokeza. Vipimo vya kupima na kutambua kuwa mtu anaye Roho wa Mungu au ana-roho zidanganyazo ni kwa kutumia neno la Mungu:

- Neno linasema lazima akiri kwamba Yesu alikuja ktk Mwili (1Yoh. 4:1)
- Neno linasema aende kwa Sheria na Ushuhuda (Isa. 8:20)
- Neno linasema kwa matunda yao mtawatambua (Math. 7:16, 20)

Wale wanaosoma maandiko wataweza kutofautisha kati ya Roho wa Mungu na roho zidanganyazo kwa uzoefu wa maandiko matakatifu. Shetani alipojigeuza ili awe kama malaika wa nuru, Yesu aliweza kumtambua na kumshinda kwa kutumia "imeandikwa."

Uwezekano wa kutambua endapo mtu ana-roho mwovu ndani yake au ana-roho wa Mungu ni kwa kutumia maandiko matakatifu. Endapo tunasoma kwa maombi na kulihifadhi neno la Mungu katika mioyo yetu, tutapewa hekima ya kupima na kutambua endapo mtu huyo anayoyadai yanatokana na Mungu au ni ya yule mwovu.

Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata **kuzigawanya nafsi na roho**, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; **tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo**.

**~ Waebrania 4:12**

## NINAWEZAJE KUMPATA ROHO MTAKATIFU MAISHANI?

Siku moja Paulo akiwa katika ziara zake za kiutume alikutana na watu ambao Biblia inasema walikuwa wanafunzi, bila shaka walikuwa wanafunzi wa Yesu. Swali la kwanza kubwa alilowauliza wale wanafunzi lilikuwa Je, mlimpokea Roho Mtakatifu mlipoamini?

akawauliza, **Je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?** Wakamjibu, La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia.
**~ Matendo ya Mitume 19:2**

Swali hili linaonyesha hawa wanafunzi walikuwa tayari wamekwisha kuamini, lakini kuna jambo kubwa zaidi lilihitajika zaidi ya kuamini. Kilichohitajika hapa ilikuwa ni kumpokea Roho Mtakatifu. Neno "mlipoamini" katika muktadha wa aya hii linamaanisha kumfahamu Mungu; au kuwa na uhakika na kutambua kuwa Mungu yupo na ya kwamba Yesu alikufa msalabani kwa ajili yao. Aina hii ya imani ni imani inayoishia katika kufahamu na kuelewa na kuwa na uhakika kwamba ndivyo maandiko yanavyosema. Imani hii haidhihiriki katika matendo, inaishia tu katika kufahamu mambo pasipo kuyatenda. Ni imani kama ile ambayo mashetani wanayo:

Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema. **Mashetani nao waamini** na kutetemeka.
**~ Yakobo 2:19**

Kwa hiyo iko aina ya imani ambayo huishia katika kufahamu lakini isiwe na matendo yanayotokana na Roho Mtakatifu. Upo uwezekano kwamba mtu anaweza akaamini na akabatizwa, lakini asimpokee Roho Mtakatifu. Ndiyo maana wamo watu ndani ya Kanisa ambao bado wanaishi maisha ya kutokukua katika mwenendo na tabia ya Kikristo: kukosekana kwa tunda la roho ni moja ya dalili kuwa mtu anaweza akawa amebatizwa lakini bado hajampokea Roho Mtakatifu.

## *Nini Maana ya Kumpokea Roho Mtakatifu?*

Tafsiri ya "kumpokea Roho Mtakatifu" (ktk Matendo 19:2), inaonekana katika lugha asilia ya Kiyunani, ni "kumshikilia" au "kumkamata." Maana yake ni kwamba tayari Mungu ametupatia Roho Mtakatifu na ndiye aliyetusaidia kuijua kweli ambayo tayari  tumeipata na ikatuongoza kufanya maamuzi ya kumpokea Yesu kama Bwana na mwokozi wa maisha yetu. Hoja aliyokuwa anaileta Paulo ni kwamba Je, baada ya kubatizwa waliendelea kumshikilia na kumkamata ili aendelee kubaki kwao? Kwa hiyo hoja ya msingi hapa ni namna gani ninaweza kuendelea kuwa na Roho Mtakatifu na kamwe nisimuache?

## *Namna ya Kuendelea Kuwa na Roho Mtakatifu*

Maandiko yanasema "yeyote ajaye kwangu sitamtupa" (Yoh. 6:37), kwa hiyo Mungu hamtupi wala hamuachi mtu, sisi ndio huwa tunamuacha na hivyo inatupasa kujifunza namna ya kubaki ndani yake na kuendelea kuacha abaki ndani yetu bila sisi kumuacha wala kumfukuza. Neno la Mungu linatuelekeza namna ya kuendelea kuishi maisha yaliyojazwa na Roho Mtakatifu:

### Ili Kumpokea Inapaswa Kuonyesha Hitaji la Kumpokea

Ikiwa ahadi haionekania kutimia kama ilivyopaswa kuonekana, ni kwa sababu ahadi haikutiliwa maanani kama ilivyopaswa. Kama wote wangemuhitaji, wote wangejazwa na Roho.[7]

### Kuendelea Kumuomba Mungu Atupatie Roho Mtakatifu

11 Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe au samaki, badala ya samaki atampa nyoka? 12 Au akimwomba yai, atampa nge? Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni **hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao**?

**~ Luka 11:13**

Mungu ameahidi kuwa wale wanaomuomba awapatie Roho Mtakatifu, atawapatia. Na katika hili ametupatia uhakika kwamba hakika atatupatia. Kila aombaye kumpokea Roho Mtakatifu hupewa Roho Mtakatifu (Math. 7:7)

Bwana yuko tayari kuwapatia Roho Mtakatifu wale wanaomtumikia Yeye kuliko jinsi wazazi walivyo tayari kuwapatia zawadi (vipawa) watoto wao. Kwa ubatizo wa kila siku wa Roho Mtakatifu kila mtendakazi anapaswa kupeleka ombi lake kwa Mungu.[8]

### Kuendelea Kujitoa kwa Mungu Kila Siku.

Asubuhi baada ya asubuhi, wakati watangazao injili watakapokuwa wakipiga magoti mbele za Bwana na kufanya upya ahadi zao za kujitoa kwake, Yeye atawapatia uwepo wa Roho Wake, unaoambatana na uamsho, na nguvu ya utakaso.[9]

Kadri mtu anavyofanya maamuzi ya kuendelea kujitoa kwa Mungu kila siku, na kuonyesha nia ya kuishi maisha ya utakatifu kila siku, ndivyo ambavyo Mungu atampatia mtu huyo Roho Mtakatifu. Zoezi hili ni la kila siku.

### Atatolewa kwa Wale Wanaomuomba Mungu Awapatie Ujumbe wa Ajili ya Jirani Zao

Roho Mtakatifu atakuja kwa wote wanaoomba mkate wa uzima ili wawapatie jirani zao.[10]

Wanafunzi hawakuomba baraka kwa ajili yao wenyewe. Walikuwa wamelemewa na mzigo kwa ajili ya mioyo. Injili ilipaswa iende mpaka miisho ya dunia, na wakadai kupokea nguvu ambayo Kristo aliiahidi. Kisha ndipo Roho Mtakatifu alipomwagwa, na maelfu waliongolewa katika siku moja.[11]

---

7 White, E. G. (1911). The Acts of the Apostles in the Proclamation of the Gospel of Jesus Christ (Vol. 4, p. 50). Pacific Press Publishing Association.

8 Ibid. p. 50.

9 Ibid. p. 56.

10 White, E. G. (1925). Instruction for Effective Christian Service (p. 252). Review and Herald Publishing Association.

11 White, E. G. (1925). Instruction for Effective Christian Service (p. 252). Review and Herald Publishing Association.

# NUKUU ZA ROHO YA UNABII JUU YA ROHO MTAKATIFU

The prince of the power of evil can only be held in check by the power of God in the third person of the Godhead, the Holy Spirit.
**Tafsiri:** Mfalme wa uovu anaweza tu kuzuiliwa kwa nguvu ya Mungu katika nafsi ya tatu ya Mungu, Roho Mtakatifu.
**~ Special Testimonies, Series A, 10:37.**

Christ gave His representative, the third person of the Godhead, the Holy Spirit.
**Tafsiri:** Kristo alitupatia mwakilishi Wake, nafsi ya tatu ya Mungu, Roho Mtakatifu."
**~ 13LtMs, Ms 44, 1898, par. 11**

Sin could be resisted and overcome only through the mighty agency of the Third person of the Godhead,
**Tafsiri:** Dhambi ingeweza kuzuiliwa na kushindwa kupitia nguvu ya nafsi ya tatu ya Mungu/Uungu
**~ Desire of Ages 671.2**

The Holy Spirit is the Comforter, in Christ's name. He personifies Christ, yet is a distinct personality....
**Tafsiri:** Roho Mtakatifu ni mfariji, katika jina la Kristo. Anamuwakilisha kristo, bali yeye ni nafsi tofauti....
**~ 20 Manuscript Release 324.2**

We need to realize that the Holy Spirit, who is as much a person as God is a person, is walking through these grounds.
**Tafsiri:** Tunahitaji kutambua kwamba Roho Mtakatifu ni nafsi, kama Mungu alivyo nafsi, naye yu atembea mahali hapa.
**~ Manuscript 66, 1899**

The Holy Spirit has a personality, else He could not bear witness to our spirits and with our spirits that we are the children of God. He must also be a divine person, else He could not search out the secrets which lie hidden in the mind of God. "For what man knoweth the things of a man, save man which is in him? even so the things of God knoweth no man, but God.
**Tafsiri:** Roho Mtakatifu anayo nafsi, vinginevyo asingeweza kuzishuhudia roho zetu na kushuhudia pamoja na roho zetu kwamba sisi ni watoto wa Mungu. Ni lazima pia awe nafsi yenye uungu, vinginevyo asingeweza kuyatafuta na kuyatambua mambo ya siri yaliyofichika katika mawazo ya Mungu. Maana ni nani awezaye kuyatambua mambo mwanadamu, isipokuwa roho iliyondani yake? Vivyo hivyo mambo ya Mungu hakuna ayajuaye, isipokuwa Mungu.
**~ Manuscript 20, 1906**

The Holy Spirit is Christ's representative, but divested of the personality of humanity, and independent thereof. Cumbered with humanity, Christ could not be in every place personally. Therefore it was for their interest that he should go to the Father, and send the Spirit to be his successor on earth. No one could then have any advantage because of his location or his personal contact with Christ. By the Spirit the Saviour would be accessible to all. In this sense he would be nearer to them than if he had not ascended on high.
**Tafsiri:** Roho Mtakatifu ni mwakilishi wa Kristo, lakini hana utu wa kibinadamu, na yuko kando nao. Akiwa amezuiliwa na ubinadamu, Kristo asingeweza kuwa kila mahali kimwili. Kwa hiyo ilikuwa ni kwa faida yao kwamba alipaswa kwenda kwa Baba, na akamtuma Roho ili awe mrithi wake hapa duniani. Sasa hakuna ambaye angeweza kupata upendeleo zaidi kwa sababu ya eneo alipopatikana au kwa sababu ya mawasiliano/mahusiano binafsi aliyikuwa nayo pamoja na Yesu. Kwa huyo Roho huyo Mwokozi angeweza kufikiwa na wote. Inamaana kwamba angekuwa karibu nao zaidi kuliko kama asingeweza kupaa juu.
**~ Review and Herald November 19, 1908, par. 3**

# Rejea


1. White, E. G. (1911). The Great Controversy Between Christ and Satan (p. 599). Pacific Press Publishing Association

2. Nichol, F. D., ed. (1980). The Seventh-day Adventist Bible Commentary (Vol. 5, p. 1037). Review and Herald Publishing Association.

3. Ibid.

4. *Provided Details

5. Nichol, F. D., ed. (1980). The Seventh-day Adventist Bible Commentary (Vol. 6, p. 1001). Review and Herald Publishing Association.

6. Ibid p. 833

7. White, E. G. (1911). The Acts of the Apostles in the Proclamation of the Gospel of Jesus Christ (Vol. 4, p. 50). Pacific Press Publishing Association.

8. Ibid. 50

9. Ibid. 56

10. White, E. G. (1925). Instruction for Effective Christian Service (p. 252). Review and Herald Publishing Association.

11. White, E. G. (1925). Instruction for Effective Christian Service (p. 252). Review and Herald Publishing Association.